

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA

Simu/Nukushi Na.025-2820068
Barua pepe: ded @mpandadc.go.tz
Tovuti: www.mpandadc.go.tz



S.L.P.1,
MPANDA

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. KTVC/MDC/S.10/22/73

05.06.2020

Wananchi wote,
TANZANIA

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Wilaya ya Mpanda anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi **Moja (1)** ya ajira ya Mkataba wa Mwaka Mmoja ya **Fundi Sanifu Ufundi na Umeme Daraja la II** kwa ajili ya kufanya kazi ya kutengeneza Magari na Mitambo mbalimbali katika Karakana ya Halmashauri kama ifuatavyo: -

1. 0. FUNDI SANIFU UFUNDI NA UMEME DARAJA LA II - NAFASI 1

1.1 Majukumu yake:

- i. Kufanya ukaguzi wa ubora wa magari ya Serikali na kurekebisha ipasavyo;
- ii. Kufanya upimaji wa mitambo na Umeme katika mtambo au gari husika;
- iii. Kufanya kazi ya kutengeneza mitambo, magari na vifaa vya umeme;
- iv. Kufanya usanifu wa miradi midogo midogo ya Umeme na kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya zinazowekwa kwenye karakana ya Ufundi na Umeme.

1.2 Sifa za Mwombaji:

Kuajiriwa wenye mojawapo ya sifa zilizotajwa hapa chini;

- i. Waliohitimu kidato cha sita (VI) na kufuzu mafunzo ya ufundi ya miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika fani ya Ufundi Mitambo/Magari (Ufundi na Umeme);
- ii. Waliohitimu kidato cha nne (IV) na kufuzu kozi ya ufundi ya miaka mitatu kutoka vyuo vya ufundi vinavyotambuliwa na Serikali katika fani ya ufundi Mitambo/Magari (Ufundi na Umeme);
- iii. Wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Hatua ya I kutoka Chuo cha Ufundi (Ufundi na Umeme) kinachotambuliwa na Serikali;
- iv. Wenye Stashahada ya kawaida katika fani ya ufundi Mitambo/Magari (Ufundi na Umeme) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

1.3 Ngazi ya Mshahara

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali yaani TGS C kwa mwezi.

NB: MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45;
2. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na taaluma vinavyohitajika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili;
3. Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa;
4. **Uwasilishaji wa vyeti vya kugushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria;**
5. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi (CV) akionesha namba za simu na anuani ya kwake na za wadhamini watatu (3);
6. Mwombaji aambatishe picha ndogo (Passport size) mbili (2) kwenye barua ya maombi;
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi;
8. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili;
9. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **19.06.2020;**
10. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta hivyo yatakayowasilishwa kwa mkono hayatapokelewa;
11. Maombi yote yatumwe kwa **njia ya posta** kwa anuani ifuatayo: -

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA,
S.L.P 01,
MPANDA**

Imetolewa na: -


Romuli Rojas John

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W'
MPANDA.**